



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA WIKI MBILI ZA MWISHO WA MWEZI
APRILI 2019

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mwelekeo wa hali ya hewa wa muda mfupi na muda wa kati kwa lengo la kuwapatia wananchi taarifa sahihi na za ziada kuhusu utabiri wa mvua iliokwishatolewa.

Maeneo mengi ya Nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara) yanatarajiwa kuendelea kuwa na upungufu wa vipindi vya mvua. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan maeneo machache ya mkoa wa Arusha. Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya ukanda wa pwani kwa wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Aprili. Kwa maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, vipindi vya mvua za kawaida vinatarajiwa kuendelea kwa kipindi chote cha mwezi kilichosalia.

Kwa maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa na Morogoro-Mahenge), Kigoma, Katavi, Tabora, Lindi na Mtwara, vipindi vya mvua za kiasi vinatarajiwa kuendelea, hata hivyo ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Lindi na Mtwara hususan wiki ya mwisho wa mwezi Aprili. Maeneo ya mikoa ya Dodoma na Singida msimu wa mvua umeisha, hivyo maeneo haya yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla.

HALI YA JOTO: Hali ya joto inatarajiwa kuwa ya kawaida katika maeneo ya pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini mashariki hususan katika kipindi cha uwepo wa mvua.

USHAURI: *Wananchi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za utabiri kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na kuzingatia tahadhari zilizotolewa na mirejeo yake pamoja na kupata na kuzingatia ushauri na miongozo ya wataalam katika sekta husika ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.*

Imetolewa tarehe 17 Aprili 2019 na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania